TANGAZO LA SERIKALI NA.676 la Tarehe 21/8/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Iimetungwa chini ya kifungu cha 7 (1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO YA MAGARI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE YA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi na Maegesho ya Magari za Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe za mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;

"ada" maana yake ni ada inayolipwa na mmiliki au dereva wa chombo cha usafiri kwa ajili ya usajili;

"chombo cha usafiri" maana yake ni gari au chombo kingine chochote kinachofanya biashara ya usafirishaji wa abiria au mizigo ndani ya eneo la Halmashauri;

"daladala" maana yake ni mabasi madogo yanayotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine ndani ya Halmashauri;

"gari" maana yake ni chombo cha usafiri chenye magurudumu manne cha binafsi au cha umma;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe;

"stendi" maana yake ni stendi ya mabasi au eneo maalumu lilolotengwa kwa ajili ya mabasi ya abiria au chombo cha usafiri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria na mizigo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote aliyeidhininishwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mpiga debe"maana yake mtu yeyote anayefanya kazi ya kutafuta abiria katika stendi ambaye si mwajiriwa wa chombo cha usafiri.

Usajili wa chombo cha usafiri

3.-(1) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri kinachofanya shughuli ya kusafirisha abiria au mizigo ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kusajili chombo hicho kwa kuwasilisha maombi ya usajili kupitia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kila mwombaji wa usajili wa chombo cha usafiri atatakiwa kulipa ada ya usajili ya mwaka kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(3) Kibali kitakachotolewa kwa mujibu wa kifungu hiki kitatakiwa kubandikwa kwenye kioo cha mbele upande wa kushoto mwa chombo cha usafiri.

(4) Mtu yeyote atakayekutwa akiendesha chombo cha usafiri ambacho kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kinapaswa kusajiliwa na Halmashauri bila ya kuwa na usajili atakuwa ametenda kosa na endapo atatiwa hatiani atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu isipokuwa tu kama atathibitisha kuwa kushindwa kusajili chombo chake kumetokana na sababu zilizo nje ya uwezo wake..

Jina na anuani ya mmiliki

4.-(1) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri atatakiwa:

(a) kuweka maamdishi katika chombo cha usafiri yanayoonyesha jina na anwani ya mmiliki kwa kadri itakavyoelekezwa na Halmashauri;

(b) kupaka rangi maalumu au alama maalumu katika chombo cha usafiri kwa kadri itakavyoelekezwa na

Halmashauri;

(c) kuwasilisha taarifa muhimu za dereva na watumishi wengine wa chombo cha usafiri kwa kadri itakavyoelekezwa na Halmashauri.

(2) Mmiliki wa chombo cha usafiri atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa na endapo atatiwa hatiani atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Maeneo ya maegesho

5.-(1) Halmashauri inaweza kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya maegesho ya vyombo vya usafiri ambayo yatakuwa nje ya hifadhi za barabara..

(2) Ada ya maegesho katika maeneo maalum yaliyotengwa itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

Stendi ya mabasi na daladala

6.-(1) Kila basi la abiria linalosafirissha abiria ndani na nje ya Halmashauri litatakiwa kuanzia safari zake au kupitia katika stendi kuu ya mabasi ya Tukuyu mjini.

(2) Kila daladala linalofanya shughuli zake ndani ya Halmashauri litatakiwa kuanzia na kumalizia safari katika stendi ya daladala iliyoainishwa na Halmashauri.

(3) Dereva wa basi au daladala atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Ushuru wa stendi

7.-(1) Kila mmiliki au dereva wa basi, daladala au chombo chochote cha usafiri kinachotumia huduma za stendi kuu ya mabasi atatakiwa kulipa ushuru wa stendi ya mabasi kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

(2) Mmiliki au dereva wa chombo chochote cha usafiri atakayeshindwa kulipa ushuru bila sababu za msingi atakuwa ametenda kosa na endapo atatiwa hatiani atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu.

Kukamata chombo cha

8.-(1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kukamata chombo chochote cha usafiri endapo mmiliki au dereva wa

usafiri

chombo hicho ataenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii.

(2) Endapo Halimashauri itakamata chombo cha usafiri kwa mujibu wa kifungu 8(1) itakitunza katika maegesho ya Halmashauri mpaka hapo mmiliki au dereva atakapoondoa upungufu uliosababisha kukamatwa kwa chombo hicho.

(3) Chombo cha usafirishaji kitakachokamatwa na kutunzwa au kuegeshwa katika maegesho ya Halmashauri kitalipiwa ada ya utunzaji ya shilingi Elfu Kumi kwa siku mpaka siku mmiliki au dereva atakapokamilisha kulipa ada au kuondoa upungufu uliosababishwa kukamatwa kwa chombo hicho.

Adhabu ya jumla

9. . Mtu yeyote atakayetenda kosa ambalo adhabu yake haijaainishwa katika Sheria Ndogo hii endapo atatiwa hatiani atahukumiwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na miwili jela na kisichozidi miezi ishirini na minne jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Uwezo wa kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote atakayekuwa ametenda kosa ambalo adhabu yake imeainishwa katika Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu thelathini na kiasi cha shilingi laki moja kwa kosa ambalo adhabu yake imeainishwa katika kifungu cha 15 endapo mkosaji atakiri kutenda kosa kwa kujaza fomu maalumu kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*(imetengenezwa chini ya kifungu cha 3(1))*

**FOMU YA USAJILI**

1. Jina kamili la Mwombaji:..............................................................
2. Kazi ya Mwombaji:...........................................................................
3. Maelezo zaidi ya gari:.......................................................................
   (a) Aina ya bodi ya gari:.................................................................

*Tangazo La Serikali Na.676 (Linaendelea.)*

(b) Rangi ya gari:............................................................................
(c) Kiwanda kilichotengeneza gari:.................................................
(d) Muundo wa gari:.......................................................................
(e) Nambari ya Injini:.....................................................................
(f) Mwaka wa kutengenezwa kwa Injini:.......................................
(g) Aina ya gari:...............................................................................
(h) Uwezo wa gari au idadi ya viti:.................................................
(i) Nambari ya leseni .....................................................................

4. Taxi au gari binafsi la kukodisha
5. Nambari ya usajiri ya gari ..............................................................
6. Kiwango cha ada ya usajili Tshs. ....................................................
7. Nambari ya Pembeni ......................................................................
8. Maegesho katika Kituo cha Mabasi ................................................

Ikiwa Mmiliki wa gari au chombo cha usafiri ataamua kuuza gari yake yake au akiamua kuacha kufanya biashara kwa mujibu wa leseni aliyopewa na Halmashauri ni sharti na lazima atoe taarifa Halmashauri haraka iwezekanavyo.

**Uthibitisho.**
Mimi .................................................... nikiwa mmiliki/dereva wa gari aina ya ..................... nathibitisha kwa maelezo niliyotoa ni kweli na sahihi kwa ufahamu wangu wote na kuwa ni kweli tupu kwa ufahamu wangu wote.

......................................
**Saini ya mwombaji**
**Tarehe .................. mwezi ................. 20...........**

**MATUMIZI YA OFISI TU.**

Maombi ya mwombaji yamekubaliwa/yamekataliwa sababu
....................................................................................................................
....................................................................................................................
....................................................................................................................
....................................................................................................................
Imetolewa leo hii tarehe .................... Mwezi ................... 20................

....................
Saini na Muhuri wa Mkurugenzi.

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 3(2))*

**ADA YA USAJILI**

| | AINA YA CHOMBO CHA USAFIRISHAJI | KIASI CHA ADA | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | Daladala au mzunguko | 70,000/= | Kwa mwaka |
| 2 | Tax Cab | 50,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Gari binafsi ya kukodishwa | 60,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Gari aina yoyote | 50,000/= | Kwa mwaka |
| 5 | Pikipiki na bajaji | 40,000/= | Kwa mwaka |
| 6 | Mkokoteni | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 7 | Baskeli za kukodisha | 10,000/= | Kwa mwaka |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 5(2))*

**USHURU WA MAEGESHO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Maegesho ya magari ndani ya Stendi zote, maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho nje ya hifadhi za barabara na masoko yote | 1,000/= | kwa siku |
| 2 | Vituo vya kuoshea magari | 6,000/= | Kwa mwezi |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1))*

**Ushuru wa kituo cha mabasi**

| Na | Aina ya chombo cha usafirishaji | Kiasi cha ada | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Basi dogo chini ya abiria 20 | Tshs. 1,000/= | Kwa siku |
| 2 | Mabasi ya kati chini ya abiria 40 | Tshs. 2,000/= | Kwa siku |
| 3 | Mabasi makubwa ya abiria zaidi ya 40 | Tshs. 4,000/= | Kwa siku |
| 4 | Lori chini ya tani 10 | Tshs. 2,000/= | Kwa siku |
| 5 | Lori zaidi ya tani 10 | Tshs. 3,000/= | Kwa siku |
| 6 | Pick up kuanzia tani moja | Tshs. 1,000/= | Kwa siku |
| 7 | Salon, tax na aina nyingine ya ma gari madogo | Tshs. 1,000/= | Kwa siku |

JEDWALI LA TANO

*Tangazo La Serikali Na.676 (Linaendelea.)*

*( Limetengenzwa chini ya kifungu cha 10)*

**FOMU YA KUFIFILISHA KOSA**

Mimi......................................................................................................... wa S.L.P ..................
Nakiri kuwa tarehe .............................. nilikiuka kifungu cha ...................... cha Sheria Ndogo ya Ushuru wa Stendi na Maegesho ya Magari ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ya Mwaka 2020.

Kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi cha Shilingi……………………na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

Leo tarehe……………………………… ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo………………………

Saini………………………………………Tarehe………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio la Mkutano Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe uliofanyika tarehe ……….. mwezi…………… 2019 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe Mbele ya Wafuatao:-

MHE. EZEKIEL M. MWAKOTA
*Mwenyekiti(W) Halmashauri Wilaya Rungwe*

BI. LOEMA I. PETER
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe*

S.L

NAKUBALI

DODOMA
5 Agosti, 2020

MHE. SELEMAN SAID JAFO
*Waziri wa Nchi, Ofisi yRais Tawala za Mikoa na Serikali Za Mitaa (TAMISEMI)*